

No. 14 Simeoni na Anna na Mtoto Yesu

© Copyright 1986, Baptist Publications House, Nairobi, Kenya, All Rights Reserved



“Mungu...alitupenda sisi na akamtuma mwanawe” (1 Yohana 4:10).

NO.14 SIMEONI NA ANNA NA MTOTO YESU

Ilikuwa siku muhimu kwa Mariamu na Yusufu. Pia, ilikuwa siku muhimu kwa mtoto Yesu. Mariamu na Yusufu walikuwa wakimpeleka mtoto Yesu hekaluni.

Yusufu alimsaidia Mariamu kuipanda juu ya punda. Alimlea mtoto Yesu walipokuwa wanasafiri. Yusufu alibeba hua wawili wa kumtolea Mungu sadaka ya shukrani.

Siku hii ilikuwa muhimu kwa Simeoni. Alikuwa mzee sana aliyeishi Yerusalemu. Alimpenda Mungu. Alimwomba Mungu. Mungu alikuwa amwemwahidi Simeoni. Alimwahidi kuwa angemwona Mwokozi.

Simeoni alijisikia kuwa ni lazima aende hekaluni. Alijisikia kuwa Mungu alimtaka aende.

Simeoni alitembea kwa haraka jinsi miguu yake ya uzee ilivyoweza. Akapanda zile hatua za hekalu. Akahisi kuwa jambo muhimu litafanyika hekaluni.

Simeoni akawaona mume na mke wakija hekaluni. Walikuwa wamembeba mtoto mchanga.

Hapo, Simeoni akajua sababu yake ya kufika hekaluni. Akajua mtoto alikuwa Mwana wa Mungu. Akauliza kama angempokea mikononi mwake. Alipomshika Yesu, akamshukuru Mungu.

“Bwana, kama ulivyoahidi. Nimemwona Mwokozi kwa macho yangu.”

Mariamu na Yusufu walistaajabia maneno haya yake. Simeoni akawaambia kuwa mtoto wao ameletwa na Mungu.

Siku hio ilikuwa ya muhimu pia kwa Anna. Alikuwa nabii mke. Alikuwa mzee sana. Aliishi hekaluni. Kila wakati alikuwa akimwomba Mungu.

Anna akawaona Mariamu na Yusufu. Akamwona Simeoni ameshika mtoto mikononi mwake. Anna alipomwona mtoto, alijua kuwa ni Yesu. Akajua Mungu alikuwa amemtuma Yesu. Anna akamshukuru Mungu. Akaanza kuwaambia wale wengine waliokuwa wakimtafuta Yesu.

Msingi wa somo ni Luka 2:22-39



"Ee Bwana wewe u Karibu" (Zaburi 119:151).

NO. 15 KUKIMBILIA MISRI

Ilikuwa wakati wa usiku huko Bethlehemu. Yesu alikuwa amelala. Mariamu na Yusufu wakawa wamelala.

Malaika akamtokea Yusufu katika ndoto. Malaika alikuwa na habari kutoka kwa Mungu. Akasema, "Yusufu, amka. Ni lazima ujitayarishe kwa safari ndefu. Mfalme anataka kumwua Yesu. Ni lazima umpeleke mbali sana. Nenda Misri. Kaa huko hadi Mungu atakapo kuambia urudi."

Yusufu akamwamsha Mariamu. Akamwambia, "Malaika ameniambia sasa hivi kuwa ni lazima tuondoke hapa. Hapa si mahali pa usalama kwa mtoto wetu. Tayarisha chakula haraka. Nami nitamleta punda."

Yusufu akamwongoza punda hadi mlangoni. Akauweka mzigo wa chakula juu ya punda. Baadaye, akamsaidia Mariamu kupanda juu ya punda. Halafu akampatia Mariamu mtoto Yesu. Yusufu alimwongoza punda kwa safari yao barabarani.

Yusufu alitembea pole pole. Yesu akalala akiwa mikononi mwa Mariamu. Wakaenda hadi nyikani. Mariamu na Yusufu walijua kwamba Mungu yu karibu. Walijua kwamba Mungu atawatunza.

Safari yao ilikuwa ndefu. Mwishowe Yusufu, Mariamu na Yesu wakafika Misri. Wakaishi huko hali wakiwa salama.


Wakati yule mfalme mwovu alipokufa, malaika alimtokea Yusufu na kumwambia, "Mnaweza mkarudi sasa."

Yusufu na Mariamu wakamrudisha Yesu nchini kwao. Walijua kwamba Mungu atawatunza. Kila wakati atakuwa yu karibu. karibu.

Msingi wa somo ni Mathayo 2:13-23.

No. 16 Mariamu na Martha

© Copyright 1986, Baptist Publications House, Nairobi, Kenya, All Rights Reserved



“Rafiki hupenda sikuzote” (Mithali 17:17).

No. 16 MARIAMU NA MARTHA

Yesu alipokuwa mkubwa, alikuwa na wasaidizi. Yesu alitaka kuwafundisha wasaidizi wake mambo mengi. Popote Yesu alipokwenda palikuwa na kusanyiko la umati mkubwa wa watu. Walimsikiliza Yesu akifundisha. Mara kwa mara waliuliza maswali. Yesu alikuwa na kazi nyingi sana.

Yesu na wasaidizi wake walisafiri mahali pengi sana. Siku moja walisafiri hadi kwa kijiji kimoja, Bethani.

Marafiki wa Yesu walikuwa wanaishi katika kijiji hiki. Akawaza, "Mariamu na Martha ni rafiki zangu. Watanikaribisha. Nitawatembelea."

Yesu alitembea kwenye njia ya vumbi hadi nyumbani kwao. Pengine Martha alimwona akija. Akamwambia Mariamu mara moja. Wakaenda kumpokea Yesu.

Martha alimletea Yesu maji baridi ya kunywa. Halafu akaanza kumtayarishia chakula. Alitaka kumfanyia rafiki yake Jesu, yaliyomema. Alitaka awe mwenye furaha.

Pia, Mariamu alifurahi kumwona Yesu. Akatembea pamoja naye. Akamwambia, "Tafadhali kaa chini na uongee nasi. Niambie mengi kuhusu upendo wa Mungu kwetu sisi wote."

Mariamu alikaa karibu na Yesu na akamsikiliza alipokuwa anaongea. Alipenda sana kusikiliza mafundisho yake.

Martha akaja na kumwambia Mariamu amsaidie. Yesu akamwambia Martha, "Unafanya kazi kwa bidii sana. Kazi unayofanya ni nzuri. Kile ambacho Mariamu anafanya ni muhimu pia."

Mara kwa mara, Yesu alipumzikia nyumbani kwao alipokuwa akisafiri. Alijua kwamba angekaribishwa nyumbani kwa rafiki zake.

Msingi wa somo ni Luka 10:38-42.

No. 17 Rafiki wa Watoto

© Copyright 1986, Baptist Publications House, Nairobi, Kenya, All Rights Reserved



"Lakini Yesu akasema, 'Waacheni watoto wadogo waje kwangu' "
(Mathayo 19:14).

No. 17 RAFIKI WA WATOTO

“Haraka! Haraka! Tusichelewe. Nataka nimwone Yesu,” akasema mvulana mdogo. Mama na baba yake walikuwa wamesikia kwamba Yesu yu karibu nao. Kwa haraka walijitayarisha kwenda kumwona Yesu.

Wanaume kwa wanawake walikuwa wanaenda kumwona Yesu. Watoto waliogeshwa na kuvalishwa nguo nzuri. Walitaka waonekane wakipendanza mbele ya Yesu.

Walipokuwa wakienda kwa haraka barabarani, baadhi ya watoto walirukaruka wengine, walikimbiakimbia. Wengine wakaimba wimbo wa furaha. Wote walifurahi kwa sababu walikuwa wanaenda kumwona Yesu.

Maua ya kupendeza yalikuwa yanakua kando kando ya barabara. Pengine wavulana na wasichana walichuma baadhi yao.

“Nataka nimpelekee Yesu na hili kama zawadi.”

“Tafadhali nataka tumwimbie Yesu wimbo.”

“Je, Yesu ni kama nani? Je, atatuambia nini?”

Watoto waliongea walipokuwa wanatembea. Wakawa wenye furaha. Akina mama na baba wakawa pia wenye furaha. Walifurahi kwa sababu watoto wao wangemwona Yesu.

Kulikuwa na umati mkubwa wa watu. Mama mmoja akasema, “Lazima hapa pawe ndipo Yesu yupo. Kuna watu wengi sana. Je, watoto watawezaje kumwona?”

Mtu mmoja akamwona mmoja kati ya wasaidizi wa Yesu. “Tafadhali waweza kutusaidia? Tunataka watoto wetu wamwone Yesu.”

“Yesu ana kazi kubwa sana. Hana nafasi ya kuongea na watoto leo. Ni lazima mrudi nyumbani,” msaidizi mmoja akawaambia.

Watoto walihuzunika sana kwa kuwa hawangeweza kumwona Yesu. Wakaanza kuondoka katika umati ule wa watu.

“Usiwafukuze watoto,” Yesu akasema. “Sina kazi nyingi. Ninataka kuwaona.”

Watoto walikusanyika karibu na Yesu. “Mungu anawapenda. Ninawapenda pia. Ninyi ni rafiki zangu,” akawaambia.

Msingi wa somo ni Mathayo 19:13-15.

No. 18 Mtoto wa Hana

© Copyright 1986, Baptist Publications House, Nairobi, Kenya, All Rights Reserved



“Namshukuru Mungu” (2 Timotheo 1:3).

No. 18 MTOTO WA HANA

Hana aliwatazama watoto walipokuwa ~~wanacheza~~ karibu na nyumba yake. Alifurahi alipowaona wakicheza pamoja.

Lakini Hana alikuwa mwenye huzuni. Kati ya wale watoto hapakuwa na wake. Hakuwa na watoto.

Hana akafikiria, "Nataka kupata mtoto. Kama ningekuwa na mtoto ningemtunza. Ningemlisha na kumwosha. Ningefundisha ampende Mungu."

Siku moja mumewe Hana akamwambia, "Nilazima twende Shilo. Ni lazima tusafiri hadi hekaluni."

Hana akaanza kujitayarisha kwa ajili ya safari. Yeye na mumewe walikuwa wanaenda hekaluni kumwabudu Mungu.

Walipofika hekaluni, Hana akaingia ndani. Akapiga magoti na kuanza kusema na Mungu. "Ninataka mtoto sana. Nitampenda. Nitamtunza. Nitamfunza akupende," akasema.

Mhubiri Eli alimwona Hana. Hakuyaelewa maneno yake. Hana akamwambia Eli kuwa ~~alikuwa~~ akiongea na Mungu. "Ninamwambia Mungu jinsi ninavyo hitaji mtoto," akasema.

Mhubiri Eli alimwona Hana. Hakuyaelewa maneno yake. Hana akamwambia Eli kuwa alikuwa akiongea na Mungu. "Ninamwambia Mungu jinsi ninavyo hitaji mtoto," akasema.

Baada ya kumwabudu Mungu, Hana na mumewe walirudi nyumbani. Hana akawa mwenye furaha. Alijua kwamba Mungu atajibu sala yake. Alijua kwamba atampatia mtoto.

Aliporudi nyumbani, Hana hakuwa mwenye huzuni tena. Alianza kujitayarisha kwa ajili ya mtoto. Alishona nguo za mtoto. Akatengeneza mahali pazuri pa mtoto kulala. Alipofanya kazi, alimshukuru Mungu kwa kujibu ombi lake.

Mtoto alipozaliwa, Hana alimwita Samweli. "Asante, Muntu, kwa mtoto wetu," Hana akomba.

Mama na baba yake Samweli walimpenda sana. Wakamtunza vizuri. Wakamfundisha kumpenda Mungu.

Msingi wa somo ni 1 Samweli 1.

No. 19 Usaidizi wa Miriamu

© Copyright 1986, Baptist Publications House, Nairobi, Kenya, All Rights Reserved



"Nitakusaidia" (Isaya 41:10).

No. 19 USAIDIZI WA MIRIAMU

Miriamu alikuwa mwenye furaha. Alikuwa na ndugu, Haruni. Alikuwa na ndugu mwingini mchanga, Musa.

Lakini Miriamu na wazazi wake walihuzunika pia. Mfalme alikuwa amewaambia askari wake kuwaua watoto wote wa kiume. Walihitajika kumficha mtoto wao ili awe salama.

Siku moja mamake Miriamu alisema, "Mtoto Musa anakua mkubwa. Analia na kucheka kwa sauti kuu. Ni lazima tutafute njia nyingine ya kumficha. Hebu nitafutie nyasi ndefu."

Miriamu alileta nyasi hizo. Mama yake akatengeneza kisafina cha manyasi. Akakipaka sifa na lami ili kisivuje.

"Miriamu, mfunike mtoto kwa blanketi. Na, niletee," mamake akamwambia.

Walimweka mtoto Musa katika kisafina hicho na kumpeleka mtoni. Walikiweka kisafina hicho kando ya mto juu ya maji. Kikaelea. Mtoto Musa alikuwa mkavu na mwenye joto.

Miriamu alijificha katika majani marefu na kukitunza kisafina hicho. Muda si muda alimsikia mtu akija. Aliogopa sana. "Je, nini kitakacho fanyika kwa mtoto huyu?" akawaza.

Miriamu akamwona bintiye mfalme na wasaidizi wake. Walikuja mtoni kuoga.

"Nileteeni kisafina hicho," malkia alimwambia kijakazi wake.

Wakati malkia alipofungua kisafina hicho, alimwona mtoto. "Huyu ni mtoto wa Kiebrania, lakini nataka nimtunze," alijiambia. "Nataka awe mtoto wangu."

Miriamu alijitokeza kutoka majanini. "Je, naweza kwenda kumtafuta mtu atakaye mtunza mtoto huyu?" aliuliza.

"Ndio, tafadhali mtafute," malkia alijibu.

Miriamu alikimbia haraka hadi kwa mama yake. "Mama njoo, malkia amempata Musa," alisema. "Anataka mtu wa kumtunza."

Miriamu na mama yake walikimbia tena hadi mtoni. Malkia akampatia mamaye Musa, mtoto wake. "Enda na mtoto huyu nyumbani na umtunze. Nitakulipa kwa kumtunza," akasema.

Miriamu na jamaa yake walifurahi sana. Mungu alikuwa amewasaidia wamtunze mtoto wao.

Msingi wa somo ni Kutoka 2:1-9.



"Tena Iweni wafadhili ninyi kwa ninyi" (Wafeso 4:32).

No. 20 AMU MWEMA

Hapo zamani za kale palikuwepo mtu ambaye alimpenda Mungu. Jina lake lilikuwa Abramamu. Alikuwa tajiri sana. Alikuwa na ngombe wengi na kondoo na mbuzi. Alikuwa na watumishi wengi wa kutunza ngombe wake.

Lutu alikuwa mpwa wa Abramamu. Aliishi na amu yake. Pia, Lutu alikuwa na ngombe wengi na watumishi wengi.

Jamaa ya Abramamu na Lutu waliishi katika mahema. Watumishi wao wote waliishi katika mahema. Waliishi katika kijiji kiitwacho Betheli.

Siku moja mtumishi alimjia Abramamu. Akamwambia, "Bwana, ngombe wa Lutu wanakula nyasi zote. Hapatakuwa na zozote za kuwalisha ngombe zetu."

"Ngombe wetu wanahitaji nyasi. Wanaweza wakakonda," akasema mmoja wa watumishi wa Lutu.

Watumishi hao wawili walianza kugombana. Walikuwa wenye hasira sana.

Abramu alimwita Lutu na wakaanza kujadiliana kuhusu jambo hili.

"Lutu, watumishi wetu wanagombana. Hivyo sio vizuri. Hakuna nyasi na maji ya kuwatosha ngombe wetu. Ni vizuri kama wewe ungeishi kivyako," Abramamu akamwambia.

"Waweza ukawapeleka jamaa yako na mifugo wako popote unapotaka. Waweza ukaenda mahali popote utakapo pamoja. Nami nitaenda kwengine. Halafu kutakuwa na nyasi za kutosha. Hakutakuwa na ugomvi tena," Abramamu akamwambia Lutu.

Lutu akainua macho yake na kutazama kila mahali. Akaona majani mabichi katika bonde la Yordani. Alijua kwamba ngombe wake watapata chakula cha kutosha.

"Nitaenda kule, Amu Abramamu. Nitawapeleka jamaa yangu na mifungo wangu katika bonde la Yordani. Kuna nyasi za kutosha."

Baadaye, Mungu alisema na Abramamu. Akamwambia, "Tazama hapo ulipo. Nitakupa yote unayoyaona sasa. Wewe na watoto wako mtaishi katika nchi hii."

"Asante, Mungu," akaomba Amu Abramamu.

Msingi wa somo ni Mwanzo 13.

No. 21 Timotheo Ajifunza

© Copyright 1986, Baptist Publications House, Nairobi, Kenya, All Rights Reserved



“Jifunzeni kutenda mema” (Isaya 1:17).

No. 21 TIMOTHEO AJIFUNZA

"Nyanya, waweza kuniambia hadithi?" Timotheo aliuliza.

Nyanya akamwambia, "Njoo, ukae karibu nami. Nitakwambia hadithi kutoka kwa karatasi za kuvingirisha za Biblia. Je, ungependa kusikia nini?" aliuliza nyanya.

"Ninapenda hadithi kuhusu Daudi," Timotheo alimjibu. "Na ninapenda hadithi nyingine pia."

Timotheo alikaa kimya na kumsikiliza nyanya yake akiongea. Alipenda sana kusikia hadithi.

Wakati mwingine mama yake Timotheo angesoma kutoka kwa karatasi za Biblia ya kuvingirisha. Timotheo alijifunza vifungu vingi sana vya Biblia. Pengine alijifunza nyimbo kuhusu marafiki wa Biblia. Timotheo alikua mkubwa akijifunza kusoma. Aliweza kusoma kurasa za Biblia ya kuvingirisha.

Timotheo alizikumbuka hadithi za Biblia. Alikumbuka vifungu vya Biblia. Yote haya yalimsadia kujua kutenda yaliyomema.

Timotheo alikua akawa mtu mkubwa. Siku moja Paulo alifika kumwona. Akamwambia Timotheo aandamane pamoja naye. Timotheo akawa msaidizi wa Paulo. Walisafiri hadi kwa miji mingi. Wakiwaambia watu kuhusu Yesu.

Baada ya ziara zao, Paulo alimwandikia Timotheo barua. Barua hizi ni sehemu ya Biblia yetu ya siku hizi.

Paulo aliandika, "Ningependa kukuona tena. Ninakumbuka jinsi ulivyompenda Mungu. Ninajua nyanya yako na mama yako walikusaidia. Walikufundisha hadithi za Biblia na vifungu vya Biblia. Walikufundisha kumpenda Mungu kila mara uyakumbuke yale waliyokufundisha.

Pengine Timotheo alisema, "Asante, Mungu. Asante kwa mama na nyanya yangu. Asante kwa Biblia na vifungu vya Biblia.

Msingi wa somo ni 2 Timotheo 1:5; 3:14-15

No. 22 Yusufu Amtii Babaye

© Copyright 1986, Baptist Publications House, Nairobi, Kenya, All Rights Reserved



“Waheshimu baba yako na mama yako” (Waefeso 6:2).

No. 22 YUSUFU AMTII BABAYE

"Yusufu, njoo hapa," Yakobo alimwita mwanawe. "Ndugu zako wanachunga kondoo na ngombe huko Skekemu. Nataka nikutume kwao. Nenda ukaone kama ndugu zako hawajambo. Halafu urudi na unilettee habari," akamwambia.

"Ndiyo, Baba," Yusufu alimjibu, "Nitafanya jinsi usemavyo."

Yusufu alijua nilazima atembee safari ndefu. Alijua angekutana na wanyama wa mwituni. Lakini alifurahi na kumtii baba yake.

Aliweka baadhi ya chakula katika kikapu. Akachukua bakora yake. Akaanza safari.

"Leo ni siku nzuri ya kutembea," akawaza Yusufu. "Mungu amecumba kila kitu vizuri."

Jua lilikuwa lenye joto jingi, lakini Yusufu hakupumzika kamwe. Alitembea, akatembea, akatembea. Mwishowe, aliyafikia yale majani mabichi.

Alifikiria pengine ndugu zake wangukuwa karibu na hapo. Hakuweza kuwaona. Aliwatafuta kila mahali, lakini hakuwapata.

"Reubeni, Reubeni," Yusufu alimwita nduguye. Halafu akasikiliza. Hakisikia jibu lo lote. Wala hakisikia sauti za kondoo. Hakuweza kuwapata ndugu zake.

Mtu mmoja alimwona. "Je, unamtafuta nani?" akamwuliza.

"Ninawatafuta ndugu zangu. Baba yangu amenituma kwao. Je, unaweza kunisaidia? Je, unajua mahali walipo?" Yusufu akamwambia.

"Wameshatoka hapa. Niliwasikia wakisema wanaenda Dothani," mtu huyo akamjibu.

"Asante sana, Bwana," Yusufu akamwambia mtu huyo.

Hata ingawa Yusufu alikuwa amechoka sana, alianza safari tena. Mwishowe akafika Dothani. Akawapata ndugu zake hapo.

Msingi wa somo ni Mwanzo 37:12-17

No. 23 Kuabudu Katika Kanisa Jipya

© Copyright 1986, Baptist Publications House, Nairobi, Kenya, All Rights Reserved



"Nitamwimbia Bwana" (Kutoka 15:1).

No. 23 KUABUDU KATIKA KANISA JIPYA

Sulemani alikuwa mfalme. Alimpelekea ujumbe rafiki yake, Hiramu.

“Ninataka kuwajengea watu wangu kanisa. Ninataka liwe kanisa la kupendeza sana. Je, unaweza kunisaidia?” akaandika Sulemani.


“Ninafurahi kukusaidia,” akamjibu Hiramu. Alimwuzia Mfalme Sulemani miti mirefu. Alikuwa na miti bora ya mwereze katika nchi yake. Sulemani aliwatuma watu wengi kwenda kuleta miti hii. Pia, walileta mawe makubwa. Walipata vifaa vilivyo bora zaidi. Iliwachukua miaka saba kujenga kanisa hilo. Mwishowe wakamaliza.

Watu wote walifika katika kanisa jipya. Mfalme Sulemani akawahutubia watu. Akawaambia, “Msifuni Mungu. Ametusaidia kulijenga kanisa hili la kupendeza.

Msingi wa somo ni I Wafalme 5-8

No. 24 Kanisa Lililo Shirikiana

© Copyright 1986, Baptist Publications House, Nairobi, Kenya, All Rights Reserved



"Leteni sadaka" (1 Mambo ya Nyakati 16:29).

No. 24 KANISA LILILO SHIRIKIANA

Paulo na Barnaba waliwatembelea washiriki wa kanisa la Antiokia. Waliwafundisha kuhusu Yesu. Wakawaambia jinsi Yesu alivyo wasaidia wengine.

Siku moja, mtu mmoja alitoka katika kanisa la Yerusalemu. Akawaambia, "Kutakuwa na njaa. Watu wengi watakuwa na njaa."

"Hapa Antiokia tuna chakula. Pengine tunaweza kusaidia marafiki zetu," mwingine akasema.

Baadhi ya watu hawa walikuwa matajiri. Walikuwa na pesa nyingi na chakula. Lakini wengine walikuwa maskini. Walikuwa tu na chakula kidogo.

Kila mtu alitoa kile ambacho aliweza. Waliokuwa na vitu vingi, walitoa vingi. Waliokuwa na vichache, nao walitoa vichache. Walipoweka zawadi zote pamoja, walikuwa wameshirikiana kutoa vitu vingi.


Waliwaambia Paulo na Barnaba wawasaidie. Wakawaambia wawapelekee zawadi zao Yerusalemu.

Watu wa Antiokia walifurahi kushirikiana. Walifurahi kwa sababu walikuwa wamesaidia marafiki zao.

Msingi wa somo ni Matendo 11:27-30

No. 25 Yesu Asoma Biblia

© Copyright 1986, Baptist Publications House, Nairobi, Kenya, All Rights Reserved



"Bwana yu mwema" (Zaburi 34:8).

No. 25 YESU ASOMA BIBLIA

Yesu alikulia katika mji mdogo wa Nazareti. Alipokua mkubwa alihama kutoka nyumbani kwao. Alijua kwamba Mungu alikuwa na jambo muhimu kwake la kufanya.

Yesu alisafiri katika miji mingi. Aliwafundisha watu kuhusu Mungu. Aliwaambia jinsi Mungu anavyowapenda.

Siku moja Yesu alirudi mjini kwao. Akaenda katika sinagogi kuabudu. Akaingia ndani na kukaa pamoja na wengine.

Yesu aliambiwa asome karatasi za kuingirisha za Biblia. Akasimama mbele ya watu. Akasome baadhi ya maandishi ya nabii, Isaya.

Isaya alikuwa ameandika kuhusu mtu maalum ambaye Mungu angemtuma. Mtu huyo angewasaidia watu. Angewaponya vipofu. Angewaambia watu kuhusu Mungu.

Yesu alipomaliza kusoma, alikunja ile karatasi ya kuingirisha ya Biblia. Alianza kusema na watu. Akawaambia, "Mimi ndimi mtu yule maalum. Mungu amenituma niwahubiria habari njema. Mungu amenituma niwasaidie. Amenituma niwaambie kuhusu upendo wake. Mimi ni mwana wa Mungu."

Watu walisikiliza kwa makini wakati Yesu alipokuwa akiongea. Wengine hawakuweza kuelewa jinsi alivyo Mwana wa Mungu. Hawakuelewa jinsi Yesu alivyokuja kuwaonyesha upendo wa Mungu.

Msingi wa somo ni Luka 4:14-22



"Nitalisifu jina la Mungu kwa wimbo" (Zaburi 69:30).

No. 26 · KUMWIMBIA YESU

Yesu na wasaidizi wake walikuwa wakienda Yerusalemu. Walipokuwa wanaufikia mji, Yesu aliwaambia, "Wawili kati yenu waende katika kijiji. Mtapata punda huko. Atakuwa na mwana punda pamoja naye. Mfungueni na mmulete kwangu."

"Mtu ye yote akiwauliza, mwambieni kwamba Bwana anambitaji. Atawakubalia ninyi kuwachukua," Yesu akawaambia.

Wasaidizi wa Yesu waliondoka mara moja. Walitembea haraka sana. Baadaye wakakifia kijiji kale. Wakatukuta punda na mwana punda. Wakawafungua. Wakampelekea Yesu.

Yesu akaanza kumpanda punda. Msaidizi mmoja akamwambia, "Yesu, hili hapa koti langu. Nitalitandika juu ya mgongo wa punda. Waweza kulikalia."

Umati mkubwa wa watu ulifika kumwona Yesu. Watu hawa walianza kutandika nguo na makoti yao barabarani. Wengine walikata matawi ya miti. Walichukua matawi hayo na kuyatandika barabarani.

Wavulana na wasichana wengi walikuwa katika umati huo. Walikuwa wamekuja kumwona Yesu. Walianza kuimba wimbo kuhusu Yesu.

"Msifuni Mungu,

Msifuni Mungu kwa ajili ya Yesu."

Watoto hawa waliimba huko wakikimbia barabarani. Waliyapunga matawi ya miti hewani. Walikimbia huku wanaimba hadi mjini. Walifurahi walipomwona rafiki yao, Yesu. Yesu alifurahi kusikia wimbo wao wa sifa.

Walipofika na kuingia mjini, baadhi ya watu waliuliza, "Je, ni nani huyu aliyemkalia punda?"

Msingi wa somo ni Mathayo 21:1-11 na Zaburi 100:1-2